

1,000,000

FEDERAL

RESERVE NOTE

1,000,000

JN 316RU4GOD

MD P 08

THE UNITED STATES OF AMERICA

ONE MILLION DOLLARS

1000000

1000000

1000000

1000000

1000000

1000000

1000000

1000000

THIS NOTE IS NOT LEGAL TENDER FOR ALL DEBTS, PUBLIC AND PRIVATE

JN 316RU4GOD

SERIES 2008 D

*Richard A. Claitor*  
Citizen of the United States

*John Calving*  
Department of Eternal Affairs

1,000,000

1,000,000

ONE

GRANT

MILLION DOLLARS

Asili ya Mungu. Biblia yasema kwamba Mungu ni mtakatifu, mkamilifu na amejitenga na viumbe vyake. Mungu anasema, "iweni watakatifu, kama nilivyo mtakatifu." Mungu anahitaji utakatifu katika mawazo, maneno, na matendo. Mungu ni mwenye haki na ameahidi kuhukumu kwa kweli. Mungu ana nguvu zote, anajua yote pia habadiliki. Huwezi kujificha au kupotosha hukumu zake za kweli. Mungu "huchunguza moyo" na ameahidi "kumlipa kila mtu kadiri ya matendo yake." Mungu ni upendo na anapenda mazuri na kuchukua mabaya. Huonea huruma "maelfu ya wenye kumpenda na kushika sheria zake" ila "hata kidogo hawezi kumrehemu mwenye hatia." Asili ya mwanadamu: Je, uko mwema? Hebu chunguza amri kumi : Je, umewahi kushuhudia uongo? "Waongo wote wanasehemu yao katika jehanamu ya moto." Je, umewahi kumtamani mtu yeyote? Yesu alisema hii ni sawa na uzinifu. Je, umewahi kumchukua mtu bila sababu? Yesu alisema hii ni sawa na uuaji. Je, umewahi kulitaja jina la Mungu bure? Mungu anasema, "Hawezi kutomuhesabia hatia alitajaye jina lake bure." Biblia inasema "Ukivunja sheria moja, una hatia kwenye yote." Mungu hakuoni kama mtu "mwema", ila anakuona kama mwongo, mzinzi, muuaji na mwenye kukufuru. "Moyo utendao dhambi, utakufa." Jehanamu (jela ya Mungu) inaelezwa kama mahala penye moto, mateso, kiza na kilio. Sababu dhambi ni kosa lisilo na mwisho zidi ya Mungu mtakatifu asiye na mwisho; jehanamu ya milele ni hukumu ya haki. Mhalifu asemapo "nimejutia", je, hakimumu atamuacha aende zake? Hata kidogo, atasema "Ni vizuri umejutia, lakini sheria inaomba uadhibiwe." Mungu ataadhibu dhambi na kujutia hakutasamehe dhambi zako. "Hakuna aliye mtakatifu; hakuna amtafutaye Mungu." Haki yetu yote ni kama vitambaa vichafu. Mtanziko mkubwa. Biblia inasema "ni vibaya sana kumtetea mtu mwovu". Sasa, Mungu mtakatifu awezaje kuwasamehe wenye dhambi wenye hatia? Msalaba = Tumaini lako la pekee. Mhalifu hawezi kujilipia faini, lakini, mtu mwingine akija na kumlipia? Hapo sheria haiwezi tena kumdai. Hii ndio Yesu aliyofanya ajili yako. Mungu alivaa mwili. Yesu aliishi maisha timilifu bila dhambi na akajitoa mwenyewe msalabani kama sadaka ajili ya upendo wake. Yesu alibeba hasira za Mungu ajili ya dhambi zako. Alikufa, akazikwa, na siku ya tatu akafufuka, ishara kwamba, adhabu ilikuwa imelipiwa. Mungu anaamuru "watu wote, mahali popote watubu" na kumuamini Yesu. Wokovu hupatikana kwa neema, kupitia imani ndani ya Yesu peke yake. Tubu, amini, mliliye Mungu. Dhambi zako zitawekwa juu ya Yesu msalabani, na haki upewe wewe. Mgeukie Mungu kwa kutubu dhambi zako na kuziacha. Muombe Mungu akupe karama yake ya toba na imani. Mliliye na kuomba rehema zake kwako. "Yeyote ajaye kwangu siwezi hata kidogo kumtupa nje." "Dhabihu za Mungu ni roho yenye kuvunjika na moyo wenye majuto." Mungu anasema, "Kwa mtu kama huyu nitaweka macho yangu, mtu aliye mnyenyekevu, mwenye moyo wa kuvunjika, na mwenye kutetemeka ajili ya neno langu. Yesu anasema "Unapaswa kuzaliwa mara ya pili." Ukiokoka utakuwa kiumbe kipya ndani ya Yesu. Utaanza kupenda vitu ulivyokuwa ukichukua, na kuchukua vitu ulivyokuwa ukivipenda. Soma Biblia kila siku na kuiheshimu. Tafuta kanisa linalohubiri Biblia. Mjulishe kila mtu kuwa umeokoka; na ukiwa umeokoka, usichukulie wokovu kama jambo la kawaida. Je, unamwamini Yesu peke yake au kazi zako? Soma waraka wa kwanza wa Yohana, na ujipime na maandiko. "Jipime uone ikiwa uko ndani ya imani." Kuna waumini wengi wa uongo Yesu atakoambia "Sijawahi kuwajua, ondokeni mbele zangu nyinyi wavunjaji sheria." Usiwe mmoja wao. "Hakikisha umeitwa na kuchaguliwa." [www.needGod.com](http://www.needGod.com)